



## TAARIFA KWA UMMA

### **KUFUNGULIWA KWA DIRISHA LA UDAHILI NGAZI YA ASTASHAHADA NA STASHAHADA KWA MWAKA WA MASOMO 2026/2027**

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) linautaarifu umma kuwa Udahili wa wanafunzi kwa mwaka wa masomo 2026/2027 kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada katika kozi zote zinazosimamiwa na NACTVET umefunguliwa rasmi leo tarehe 28 Mei, 2026.

Maombi ya udahili kwa kozi za Afya na Sayansi Shirikishi -Tanzania Bara, yatafanyika kupitia Mfumo wa Udahili wa Pamoja (Central Admission System – CAS) unaopatikana katika tovuti ya Baraza ([www.nactvet.go.tz](http://www.nactvet.go.tz)) kuanzia tarehe 28 Mei hadi tarehe 10 Julai, 2026 kwa awamu ya kwanza.

Aidha, maombi ya kozi zisizo za Afya na Sayansi Shirikishi, na kozi za Afya na Sayansi Shirikishi zitolewazo katika vyuo vilivyoko Zanzibar yatumwe moja kwa moja kwenye vyuo husika kuanzia tarehe 28 Mei hadi tarehe 10 Julai, 2026 kwa awamu ya kwanza.

Baraza pia linautaarifu umma kuwa orodha ya kozi zote na vyuo vinavyotoa kozi hizo, inapatikana katika Kitabu cha Mwongozo wa Udahili kwa Mwaka wa Masomo 2026/2027 (Admission Guidebook for Academic Year 2026/2027). kinachopatikana katika tovuti ya Baraza ([www.nactvet.go.tz](http://www.nactvet.go.tz)).

Baraza linasisitiza kila mwombaji kuhusika mwenyewe katika zoezi zima la kuomba kudahiliwa, kuandika taarifa zake kwa usahihi na umakini, na kutunza kumbukumbu atakazopatiwa na Baraza kupitia namba yake ya simu, bila kumpatia mtu mwingine yeyote ili kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza katika zoezi zima la maombi ya kujiunga na kozi katika vyuo mbalimbali.

Mambo ya Kuzingatia kwa Wanaoomba Kupitia Mfumo wa Udahili wa Pamoja (Central Admission System – CAS):

1. Mwombaji anaweza kuomba chuo zaidi ya kimoja. Kuchaguliwa katika chuo alichooomba kutategemea ushindani utakaokuwepo katika chuo hicho.
2. Mwombaji akishachaguliwa, atapokea ujumbe kutoka NACTVET kupitia namba yake ya simu aliyoweka kwenye mfumo wakati wa kufanya maombi. Ujumbe huo utamjulisha kuwa amechaguliwa kujiunga na chuo fulani (jina la chuo), na utakuwa na msimbo (code) ambao atatakiwa kuutunza na kuuwasilisha kwa chuo alichochaguliwa siku atakapowasili chuoni kwa ajili ya kuanza masomo.
3. Baada ya kuwasilisha msimbo huo chuoni, atasajiliwa na chuo, kisha atapokea ujumbe kutoka NACTVET ukimweleza kuwa amesajiliwa.
4. Baada ya kusajiliwa, mwanafunzi aingie katika tovuti ya NACTVET ([www.nactvet.go.tz](http://www.nactvet.go.tz)), kisha ajiridhishe kuwa amesajiliwa kwa kuhakiki taarifa zake kwa kubonyeza “link” inayosomeka “student’s information verification”.

Mambo ya Kuzingatia kwa Wanaoomba Moja kwa Moja Vyuoni:

1. Mwombaji anaweza kuomba chuo zaidi ya kimoja. Kuchaguliwa katika chuo alichooomba kutategemea ushindani utakaokuwepo katika chuo hicho.
2. Mwombaji akishachaguliwa na chuo, chuo husika kitawasilisha taarifa za mwombaji NACTVET kwa ajili ya uhakiki. Mwombaji atapokea ujumbe ukimtaarifu kuwa taarifa zake zimewasilishwa NACTVET na chuo kwa ajili ya kuhakikiwa.
3. Baada ya taarifa zake kuhakikiwa, atapokea ujumbe kutoka NACTVET ukimjulisha kuwa amehakikiwa, na utakuwa na msimbo (code) ambao atatakiwa kuutumia kuangalia taarifa zake za uhakiki. Pia atatakiwa kuutunza msimbo huo na kuuwasilisha kwa chuo alichochaguliwa siku atakapokwenda katika chuo hicho kwa ajili ya kuanza masomo.

4. Baada ya kuwasilisha msimbo huo chuoni, atasajiliwa na chuo, kisha atapokea ujumbe kutoka NACTVET ukimueleza kuwa amesajiliwa.
5. Baada ya kusajiliwa, mwanafunzi anatakiwa aingie katika tovuti ya NACTVET ([www.nactvet.go.tz](http://www.nactvet.go.tz)), kisha ajiridhishe kuwa amesajiliwa kwa kuhakiki taarifa zake kwa kubonyeza “link” inayosomeka “Student’s information verification”.

Vyuo vyote vinakumbushwa kuzingatia kikamilifu Kanuni, Miongozo na Taratibu zilizowekwa na Baraza.

